MFUKO WA MISITU TANZANIA

Kwa Kudumisha Ugharimiaji wa Usimamizi wa Misitu

Tangazo la Kuitisha Maandiko ya Miradi la Mwaka 2017

Utangulizi:

Mfuko wa Misitu Tanzania (TaFF) umeanzishwa kisheria (chini ya Sheria ya Misitu Sura 323 ya mwaka 2002), kama njia endelevu ya kuwezesha uhifadhi, usimamizi na uendelezaji wa rasilimali misitu katika Mikoa yote ya Tanzania Bara. Mfuko huu umeanzishwa kwa lengo la kukabiliana na changamoto za usimamizi wa rasilimali ya misitu hasa katika kuimarisha utekelezaji wa Sera na Sheria ya Misitu. Mfuko wa Misitu Tanzania ni Mfuko wa Umma uliopo chini ya Wizara ya Maliasili na Utalii, na ulianza rasmi utekelezaji wa majukumu yake Julai 2011.

Kwa mujibu wa kifungu cha 80 cha Sheria ya Misitu Sura 323 ya mwaka 2002, Majukumu makuu ya Mfuko wa Misitu Tanzania ni:

(i) Kuwezesha uhamasishaji wa jamii kupitia elimu na mafunzo kwa Umma juu ya umuhimu wa uhifadhi, uendelezaji na matumizi endelevu ya rasilimali misitu;

(ii) Kuwezesha uendelezaji wa misitu ya jamii kwa kutoa misaada na ushauri kwa vikundi, watu binafsi na wadau wengine wanaojihusisha na uhifadhi, uendelezaji na usimamizi wa rasilimali misitu;

(iii) Kukuza, kuendeleza na kufadhili utafiti wa misitu;

(iv) Kusaidia na kuwezesha Tanzania kunufaika na Mipango na Mifuko ya Kitaifa na Kimataifa iliyopo kwa nia ya kuhifadhi na kulinda bioanuwai, na kuhifadhi na kuendeleza rasilimali misitu;

(v) Kusaidia na kuwesesha vikundi na watu binafsi kushiriki katika midahalo na mijadala inayohusu masuala ya misitu na masuala yanayohusiana na uandaaji wa tathmini za kimazingira;

(vi) Kusaidia na kuwezesha usimamizi na utekelezaji wa Sheria ya Misitu, Kanuni zake na miongozo husika; na

(vii) Kukuza na kuwezesha shughuli nyingine zinazoendana na majukumu ya Mfuko wa Misitu Tanzania yaliyoainishwa kwenye kifungu cha 80 cha Sheria ya Misitu Sura 323 ya mwaka 2002 na shughuli zinazohusiana na madhumuni ya Sheria ya Misitu Sura 323 ya mwaka 2002.

Mfuko wa Misitu Tanzania unashirikisha wadau katika kutekeleza majukumu yake, na utoaji wa ruzuku ni njia mojawapo ya ushirikiswaji wa wadau. Kwa sababu hiyo basi, Mfuko wa Misitu Tanzania unatoa **Tangazo la Kuitisha Maandiko ya Miradi.**

Wanaoweza kuomba Ruzuku

Maandiko ya miradi ya kuomba ruzuku inayotolewa na Mfuko wa Misitu Tanzania yanakaribishwa kutoka kwa watu binafsi, vikundi vya jamii, asasi zisizo za kiserikali, jumuiya/taasisi za kidini, asasi/taasisi za mafunzo, taasisi za utafiti, wizara, idara, na wakala za serikali, mamlaka za serikali za mitaa na wadau wengine wanaojihusisha na uhifadhi, usimamizi na uendelezaji wa rasilimali misitu katika Mikoa ya Tanzania Bara. Hata hivyo, vikundi/asasi/taasisi zote zitakazowasilisha maandiko ya miradi zinatakiwa ziwe zimesajiliwa na mamlaka zinazotambulika kisheria. Kwa sababu hiyo basi, nakala za nyaraka zinazothibitisha kuwa vikundi/asasi/taasisi husika imesajiliwa zinatakiwa kuambatishwa kwenye andiko la miradi. Aidha, waombaji binafsi wanatakiwa kuwasilisha barua kutoka kwa wadhamini wawili au zaidi wanaoaminika na wanaotambulika kisheria, na mdhamini mmoja ni lazima awe Mtendaji wa Kijiji/Mtaa anaoishi mwombaji wa ruzuku, na iwapo sehemu mradi utapotekelezwa ni tofauti na sehemu anakoishi mwombaji wa ruzuku, barua ya udhamini kutoka kwa Mtendaji wa Kijiji/Mtaa ambako mradi utatekelezwa inapaswa pia kuwasilishwa.

Maeneo ya Kipaumbele Yanayozingatiwa katika Utoaji wa Ruzuku

Mfuko wa Misitu Tanzania utatoa ruzuku katika maeneo matatu ya kipaumbele kama ifuatavyo:

(i) Uhifadhi, Usimamizi na Uendelezaji wa Rasilimali Misitu;

(ii) Uboreshaji wa Maisha ya Jamii zinazoishi Pembezoni mwa Misitu, hasa Misitu ya hifadhi; na

(iii) Utafiti Tumizi na Rekebu katika Masuala ya Misitu.

Maeneo Yanayoweza Kupatiwa Ruzuku katika Vipaumbele Vitatu vya TaFF

Kwa kuzingatia vipaumbele vitatu vya TaFF vilivyoainishwa hapo juu, baadhi ya maeneo yatayofikiriwa kupatiwa ruzuku yamefafanuliwa hapo chini. Hata hivyo, kwa mwaka 2017 wadau wote wataowasilisha maandiko ya miradi ya utafiti, ni lazima wazingatie maeneo ya utafiti yaliyotajwa chini ya eneo la kipaumbele la utafiti tumizi na rekebu katika masuala ya misitu na sio vinginevyo. Hii inamaanisha kuwa maandiko yote ya miradi ya utafiti ambayo hayatazingatia maeneo hayo ya utafiti yaliyotajwa chini ya eneo la kipaumbele la utafiti tumizi na rekebu katika masuala ya misitu **hayatakubalika**.

1. **Baadhi ya Maeneo Yanayoweza Kupatiwa Ruzuku chini ya Kipaumbele cha Uhifadhi, Usimamizi na Uendelezaji wa Rasilimali Misitu ni:**
   (i) Usimamizi na matumizi endelevu ya rasilimali misitu.
   (ii) Ubainishaji na uwekaji wa mipaka ya misitu.
   (iii) Usimamizi shirikishi wa misitu.
   (iv) Uanzishwaji wa vitalu vya miti na upandaji miti.

2. **Baadhi ya Maeneo Yanayoweza Kupatiwa Ruzuku chini ya Kipaumbele cha Uboreshaji wa Maisha ya Jamii zinazoishi Pembezoni mwa Misitu, hasa Misitu ya hifadhi ni:**
   (i) Kuongeza thamani na utafutaji wa masoko ya mazao ya misitu.
   (ii) Uendelezaji wa mazao ya misitu yasiyo ya mbao na ukuzaji wa matumizi yake.
   (iii) Ufugaji nyuki na shughuli nyingine za kuboresha kipato cha jamii ambazo ni rafiki wa mazingira.
   (iv) Uanzishwaji wa vitalu vya miti na upandaji miti.

3. **Maeneo Pekee ya Utafiti Yatakayofikiriwa Kupatiwa Ruzuku chini ya Kipaumbele cha Utafiti Tumizi na Rekebu katika Masuala ya Misitu** yameainishwa hapo chini. Hata hivyo, kwa kuwa masuala ya utafiti ni ya kitaalam na yanawahusu watafiti kutoka taasisi za utafiti na

vyuo vya mafunzo vinavyofanya utafiti, maeneo ya utafiti yamebaki kwa lugha ya Kiingereza kama yalivyoainishwa hapo chini:

Theme 1: Plantation forestry and tree improvement

Sub-themes under this theme are as follows:

i) Search for new plantation tree species with emphasis on indigenous species.

ii) *Assess effects of forest plantations on water resources, biodiversity and soil health*.

Theme 2: Forestry resource assessment

Sub-theme under this theme is as follows:

i) Develop simple forest resource assessment methods for local communities.

Theme 3: Community and farm forestry

Sub-themes under this theme are as follows:

i) Undertake biological evaluation of various Agroforestry technologies for various end uses in sets of ecological zones and farming systems.

ii) Assess and provide/develop management techniques/guidelines for woodlots and tree outside the forests (ToF).

Aina za Ruzuku Inayotolewa na Mfuko wa Misitu Tanzania

Mfuko wa Misitu Tanzania unatoa ruzuku za aina tatu ambazo ni kama ifuatavyo:

(i) **Ruzuku Ndogo:** kiasi cha fedha kisichozidi Shilingi za Kitanzania (TZS) milioni tano (5).

(ii) **Ruzuku ya Kati:** kiasi cha fedha kinachozidi TZS milioni tano (5) lakini haizidi TZS milioni 20.

(iii) **Ruzuku Kubwa:** kiasi cha fedha kinachozidi TZS milioni 20 lakini haizidi TZS milioni 50.

Aina ya uwezeshaji Unaotolewa na Mfuko wa Misitu Tanzania

Mfuko wa Misitu Tanzania utatoa aina tatu za uwezeshaji ambazo ni:

(i) **Uwezeshaji wa Fedha:**Waombaji wa ruzuku wanaweza kupatiwa fedha kwa ajili ya kugharimia shughuli zilizoidhinishwa;

(ii) **Uwezeshaji wa Vifaa:** Waombaji wa ruzuku wanaweza kupata vifaa kama vile nyenzo na vitendea kazi; na

(iii) **Uwezeshaji wa Stadi/Utaalam**: Mfuko wa Misitu Tanzania unaweza kuwezesha huduma ya stadi/utalaam kulingana na mahitaji ya waombaji wa ruzuku.

Vigezo Vinavyotumika Wakati wa Kuchagua Miradi

Maandiko ya miradi ambayo yatafikiriwa kupatiwa ruzuku ya Mfuko wa Misitu Tanzania yanapaswa kutimiza vigezo vifuatavyo:

(i) Andiko la mradi lionyeshe kuwa utekelezaji wa mradi utachangia katika uhifadhi na usimamizi wa rasilimali misitu;

(ii) Andiko la mradi lionyeshe kuwa mradi unatoa faida ya moja kwa moja au isiyo ya moja kwa moja kwa walengwa;

(iii) Shughuli zitakazotekelezwa ziwe wazi na kuwepo na uwajibikaji;

(iv) Andiko la mradi lionyeshe kuwepo kwa ubunifu;

(v) Andiko la mradi lionyeshe kuwa matokeo ya utekelezaji wa mradi yatatumika kuboresha usimamizi wa rasilimali misitu;

(vi) Andiko la mradi lithibitishe uwezo wa mwombaji wa kufanikisha malengo na shughuli zilizopendekezwa;

(vii) Andiko la mradi lithibitishe uwezo wa mwombaji wa kutekeleza na kusimamia shughuli za mradi;

(viii) Andiko la mradi lionyeshe kuwa kuna uendelevu wa shughuli za mradi zitakazotekelezwa;

(ix) Ushiriki wa wadau;

(x) Mwombaji wa ruzuku ya kati na kubwa aahidi kuwa atachangia asilimia 20 (fedha au hali na mali) ya jumla ya fedha yote inayoombwa;

(xi) Andiko la mradi lithibitishe uwepo wa watumishi wenye ueledi wa aina ya mradi ulioombwa ili kurahisisha utekelezaji; na

(xii) Andiko la mradi lionyeshe kuwa mradi utatekelezwa katika Mikoa ya Tanzania Bara.

Maandiko yote ya miradi ambayo yatafanana au yatakuwa na vipengele vinavyofanana huwa hayatapendekezwa kupatiwa ruzuku kwa kuwa ni vigumu kutofautisha andiko la mradi lililoandaliwa na andiko la mradi lililonakiliwa kutoka maandiko mengine.

Upokeaji wa Maandiko ya Miradi

Mwisho kupokea maandiko ya miradi inayoomba ruzuku ndogo ni tarehe 30 Juni na 31 Desemba wakati mwisho wa kupokea maandiko ya miradi inayoomba ruzuku ya kati na ruzuku kubwa ni

tarehe 31 Machi. Maombi yoyote yatakayowasilishwa baada ya tarehe ya mwisho ya kupokea maandiko ya miradi hayatashughulikiwa.

Uwasilishaji wa Maandiko ya Miradi

Waombaji wa ruzuku watawasilisha nakala 2 za maandiko ya miradi (nakala ya kielektroniki au nakala ya kine) kwenye ofisi ya Mfuko wa Misitu Tanzania. Nakala ya kine itawasilishwa kwa njia ya posta wakati nakala ya kielektroniki itawasilishwa kupitia anwani ya baruapepe ya Mfuko ambayo ni info@forestfund.go.tz Hata hivyo, nakala ya kielektroniki ni lazima iwe kwenye muundo wa PDF. Sekretarieti ya Mfuko wa Misitu Tanzania itawajulisha waombaji kuhusu kupokelewa kwa maandiko yao ya miradi.

Maandiko yote yaelekezwe kwa:

Katibu Tawala,
Mfuko wa Misitu Tanzania,
S.L.P. 11004,
***Dar es Salaam**.*
Simu: +255 (0) 222865816
Faksi: +255 (0) 222865165
baruapepe: info@forestfund.go.tz
Tovuti: www.forestfund.go.tz

Muundo na Maandiko ya Miradi

Maandiko yote ya miradi inabidi yanapaswa kutayarishwa kwa kuzingatia miundo ya Mfuko. Maandiko ya ruzuku ndogo yanatakiwa yafuate muundo ulioneshwa kwenye Kiambatisho Na. 2. Maandiko ya ruzuku ya kati na ruzuku kubwa yatafuata muundo ulioneshwa kwenye Kiambatisho Na. 3. Maandiko ambayo hayarandani na miundo iliyotajwa hayatakubaliwa. Maandiko yasizidi kurasa 15 ukiondoa viambatisho.

Kiambatisho Na. 2: Muundo wa Andiko la Mradi kwa ajili ya Ruzuku Ndogo

1.0 **Taarifa za Msingi kuhusu andiko la Mradi**

1.1 Jina la Mradi:
1.2 Jina na Anwani ya Mwombaji:
1.3 Jina na sifa za Muunganishi:
1.4 Mahali Mradi utakapotekelezwa:
1.5 Eneo la kipaumbele la Mfuko wa Misitu Tanzania:
1.6 Aina ya Ruzuku:
1.7 Aina ya Uwezeshwaji:
1.8 Jumla ya gharama ya Mradi (Sh.):
1.9 Jumla ya kiasi kinachoombwa kutoka Mfuko wa Misitu Tanzania (Sh):
1.10 Michango mingine ikiwemo ya Hali na Mali:
1.11 Muda wa Utekelezaji wa Mradi na Mwezi ambao Utekelezaji utaanza:

2. Usuli wa Mradi:
3. Mantiki na Uthibitisho wa Mradi:
4. Malengo ya Mradi na Viashiria vya Utendaji:
5. Matokeo yatarajiwayo kutoka kwenye Mradi:_____
_____
6. Shughuli mahususi zitakazotekelezwa ili kufikia matokeo:_____
_____
7. Watakaonufaika na Mradi:_____
_____
8. Hatua au mbinu zitakazotumika ili kufikia malengo:_____
_____
9. Watumishi wa mradi na ueledi wao

Mwombaji aonyeshe idadi ya watumishi na ueledi wao kwenye andiko la mradi ili kurahisisha na kufanikisha utekelezaji wa mradi husika _____

10. Ratiba ya utekelezaji wa Mradi:_____
_____

11. **Bajeti ya Mradi**

Mwombaji wa ruzuku atatakiwa kugawanya bajeti ya mradi wake katika awamu mbili. Hata hivyo, 10% ya fedha za awamu ya pili itabakizwa hadi taarifa ya kukamilisha mradi itakapowasilishwa na kukubalika. Mgawanyo wa fedha za ruzuku ni kama ifuatavyo: 50% (fedha za awamu ya kwanza), 50% kutoa 10% ya fedha itakayobakizwa (fedha za awamu ya pili) na 10% ya fedha za awamu ya pili (fedha itakayobakizwa). Bajeti ya mradi (pamoja na mchanganuo wa kila kipengele) inayojumuisha michango mingine ya hali na mali na thamani yake ifuate yaliyodokezwa kwenye Jedwali la 2.

Jedwali la 2: Kiolezo cha Bajeti ya Ruzuku Ndogo

Kipengele (Shughuli)	Kizio	Kiasi	Gharama ya kizio (Sh)	Jumla ya Gharama(Sh)
	Jumla			
	Kiasi kinachoombwa toka Mfuko			
	Michango kutoka kwa wengine			
	Mchango wa Mwombaji			

RIDHAA:

12. Maoni na Mapendekezo ya Mkuu wa Taasisi/Asasi:
    _____
    Jina:_____Cheo:_____Muhuri rasmi:_____
    Saini:_____Tarehe:_____
    Maoni:_____
    Jina:_____Cheo:_____Muhuri rasmi:_____
    Saini:_____Tarehe:_____

13. Maoni na Mapendekezo ya Kijiji/ Mtendaji wa Mtaa ambapo Mradi utakapotekelezwa.

    Maoni:_____
    Jina:_____Cheo:_____Muhuri rasmi:_____
    Saini:_____Tarehe:_____

14. Maoni na Mapendekezo ya Mkurugenzi wa Halmashauri ambapo mradi utakapotekelezwa:

    Maoni:_____
    Jina:_____Cheo:_____Muhuri rasmi:_____
    Saini:_____Tarehe:_____

Kiambatisho Na. 3: Muundo wa Andiko la Mradi kwa ajili ya Ruzuku ya Kati na Kubwa

UTANGULIZI

(i) Kabla ya kujaza maombi haya, tafadhali soma vigezo vya ustahili na madhumuni ya wito wa maandiko ya miradi ili kuhakiki iwapo mradi wako unazo sifa za kufikiriwa kupatiwa ruzuku na Mfuko.
(ii) Tafadhali wasilisha fomu ya maombi ukitumia muundo na maelekezo yaliyotolewa ama sivyo maombi hayatakubaliwa.
(iii) Maombi yawasilishwe kabla ya mwisho wa saa za kazi ya tarehe ya mwisho. Tarehe ya mwisho ni tarehe ambayo maombi ya ruzuku yawe yamepokelewa na Sekretarieti. Maombi yatakayowasilishwa baada ya tarehe ya mwisho hayatashughulikiwa.
(iv) Maandiko yawe nadhifu, mepesi kusomeka na yawe na fonti ya pointi 12 na nafasi kati ya sentensi ya 1.5.
(v) Mwombaji aonyeshe idadi ya watumishi na ueledi wao kwenye andiko la mradi ili kurahisisha na kufanikisha utekelezaji wa mradi husika.
(vi) Mwombaji atatakiwa kugawanya bajeti ya mradi wake katika awamu tatu kwa kuzingatia asilimia arobaini (40%) fedha za awamu ya kwanza, asilimia thelathini (30%) fedha za awamu ya pili na asilimia thelathini (30%) fedha za awamu ya tatu.
(vii) Mwombaji yeyote mwenye maswali au hoja awasiliane na Mfuko.

1.0 TAARIFA ZA MSINGI KUHUSU ANDIKO LA MRADI

1.1 Jina la Mradi: .....
1.2 Jina na Anwani ya Mwombaji: .....
1.3 Jina na sifa ya Muunganishi: .....
1.4 Mahali Mradi utakapotekelezwa : .....
1.5 Eneo la kipaumbele la Mfuko wa Misitu Tanzania: .....
1.6 Aina ya Ruzuku inayoombwa:.....
1.7 Aina ya uwezeshwaji unaoombwa:…….
1.8 Mantiki na uthibitisho wa kuwa na Mradi (yasizidi maneno 250)
1.9 Malengo ya Mradi na viashiria vya utendaji
1.10 Matokeo yanayotarajiwa kutoka kwenye Mradi
1.11 Watakaonufaika na Mradi
1.12 Jumla ya kiasi kinachoombwa kutoka kwenye Mfuko (Sh):
1.13 Michango mingine ikiwemo ya hali na mali (Sh):
1.14 Muda wa Utekelezaji wa Mradi na mwezi ambao utekelezaji utaanza:

2. RIDHAA

(a). Mapendekezo ya Mkuu wa Taasisi zinazo/inayoomba

Maoni:_____

Jina:_____Cheo:_____Muhuri rasmi:_____

Saini:_____Tarehe:_____

(b) Mapendekezo ya Kijiji/ Mtendaji Kata/ Mtaa (ambapo Mradi utakapotekelezwa).

Maoni:_____

Jina:_____Cheo:_____Muhuri rasmi:_____

Saini:_____Tarehe:_____

(c) Mapendekezo ya Mkurugenzi wa Halmashauri utakapokuwa Mradi:

Maoni:_____

Jina:_____Cheo:_____Muhuri rasmi:_____

Saini:_____Tarehe:_____

3.0 MATINI KUU

3.1 Muhtasari wa Mradi

Muhtasari wa mradi unatakiwa kuwa na sehemu muhimu zote za Mradi ulioandikwa ikiwemo ya matatizo yanayokusudiwa kutatuliwa, malengo, matokeo yanayotarajiwa, mantiki na uthibitisho wa mradi, shughuli kuu zitakazofanyika, matumizi ya matokeo ya mradi katika kuendeleza uhifadhi na usimamizi wa rasilimali misitu. Muhtasari usizidi maneno 250 na ueleweke kwa watu wengine wafanyao kazi kwenye taaluma hiyo au taaluma zenye uhusiano wa karibu nayo na pia ueleweke kwa wale ambao siyo wa mchepuo huo.

3.2 Utangulizi

Utangulizi uiweke mada bayana au tatizo linalokusudiwa kutatuliwa na utoe mtazamo wa jumla wa mradi ulioandikwa, muktadha wake ndani ya eneo husika la kipaumbele na taarifa kuhusu jitihada zilizokwisha fanywa au zinazoendelea kufanywa katika kuishughulikia mada.

3.3 Azma na Madhumuni ya Mradi na Matokeo Yanayotarajiwa

Mwombaji anatakiwa kufafanua azma ya Mradi akionesha bayana jinsi utakavyochangia katika usimamizi wa rasilimali misitu kwenye eneo la utekelezaji wa mradi. Ni muhimu kueleza madhumuni na matokeo yatakayopatikana kutokana na utekelezaji wa shughuli zilizopendekezwa. Taarifa pia ionyeshe jinsi mradi unaopendekezwa utakavyoimarisha jitihada za kuboresha maisha ya jamii, ushiriki na ufahamu wao wa usimamizi urari wa rasilimali misitu. Mikakati ya kusambaza

matokeo ya mradi pia iwekwe wazi. Sehemu hii pia ieleze watakaonufaika na mradi na jinsi watakavyonufaika na utekelezaji wake. Ili kurahisisha mapitio na uperembaji wa Mradi, mwombaji anatakiwa kutoa Jedwali lijengalo hoja yenye mantiki **ya** kukubalika kwa mradi. Hii inafanywa kwenye safu na misafa vinavyoonesha malengo na shughuli za kila lengo, matokeo yanayotarajiwa na athari zake. Ratiba ya utekelezaji ionyeshe bayana shughuli zitakazofanyika ili kuzisaidia pande zote katika uperembaji wa maendeleo ya mradi na kurekebisha ratiba na bajeti ipasavyo.

3.4 Mbinu za Kutekeleza Mradi

Katika sehemu hii mwombaji wa ruzuku anatakiwa aweke bayana jinsi anavyotarajia kufanikisha malengo ya mradi na matokeo yanayokusudiwa. Shughuli za mradi zinazokusudiwa kufanywa zinatakiwa zielezwe kikamilfu na mpango wa kazi utayarishwe. Aidha, michango ya wadau wengine katika utekelezaji wa mradi ni lazima iwekwe bayana.

3.5 Vichocheo Vikuu vya Mafanikio

Mwombaji aeleze na kuchambua vichocheo vikuu ambavyo vitaathiri mafanikio ya mradi na jinsi ya kuhakikisha kuwa vichocheo hivyo vimewekwa. Uchambuzi wa vichocheo hivyo unatakiwa utilie maanani muktadha wa mradi mzima na uwezo wa watekelezaji.

3.6 Mpango wa Uperembaji na Tathmini

Sehemu hii itaeleza jinsi mradi utakavyofanyiwa uperembaji na tathmini katika kipindi chote cha utekelezaji. Kuwepo na maelezo ya parameta/vigezo vinavyopimika ambavyo vitaainisha iwapo shughuli zilizopangwa zitaleta mabadiliko kwenye tatizo au suala ambalo mradi umelenga. Pia, mwombaji atoe ufafanuzi unaohusu jinsi ya kupima mafanikio ya mradi. Ni muhimu pia kutambua kuwa jedwali lijengalo hoja yenye mantiki iletayo kukubalika kwa mradi; lenye safu na misafa vinavyoonesha malengo, shughuli zake, n.k. (Tazama 2.3) linatakiwa kutayarishwa ili kusaidia uperembaji wa utekelezaji wa mradi.

3.7 Mpango Endelevu wa Mafanikio ya Mradi

Sehemu hii ieleze jinsi mafanikio yatavyodumishwa baada ya mradi kumalizika. Andiko la mradi halina budi kuonyesha jinsi mradi au mchakato utakaoanzishwa utakavyoendelezwa baada ya kipindi cha mradi na ruzuku ya Mfuko kumalizika.

3.8 Bajeti

Bajeti ni sehemu muhimu ya ombi la ruzuku, hivyo bajeti ya kutekelezea andiko la mradi inatakiwa:

(i) iwe ina uhalisia na inayokubalika;

(ii) ieleze kila kipengele kikamilifu;

(iii) iwe inayoeleweka kwa urahisi;

(iv) iwe na hesabu sahihi; na

(v) izingatie ukweli na iwe inayoweza kutetewa.

Bajeti ifafanuliwe kwa kila kipengele kuonyesha wazi kiasi kilichoombwa kutoka Mfuko, kiasi kutoka vyanzo vingine, na mchango wa Mwombaji. Inasisitizwa kuonesha michango ya hali na mali kuwa ni sehemu ya gharama ya mradi. Bajeti inatakiwa kuwa na maelezo yanayoonesha jinsi kila kiasi kilivyokokotolewa (gharama ya vizio) na uhitaji na matumizi kwa kila kipengele. Vipengele vifuatavyo visioneshwe kwenye bajeti kwani havitagharimiwa na Mfuko: mishahara ya watumishi, ununuzi wa magari, tunzo na gharama nyingine ambazo hazihusiani moja kwa moja na mradi. Hata hivyo, waombaji watambue kuwa baada ya bajeti kupitishwa, manunuzi ya vifaa yanatakiwa yatokane na ankara za uwianisho wa bei kutoka kwa watoa huduma wasiopungua watatu au kwa kufuata Sheria na Kanuni za Manunuzi ya Umma ya mwaka 2004. Wakati mwingine Mfuko unaweza kununua vifaa vinavyotakiwa badala ya kutoa fedha taslimu kwa Mwombaji. Mwombaji atatakiwa kugawanya bajeti ya mradi wake katika awamu tatu kwa kuzingatia asilimia arobaini (40%) fedha za awamu ya kwanza, asilimia thelathini (30%) fedha za awamu ya pili na asilimia thelathini (30%) fedha za awamu ya tatu. Bajeti ya mradi (pamoja na mchanganuo wa kila kipengele) inayojumuisha michango mingine ya hali na mali na thamani yake ifuate yaliyodokezwa kwenye Jedwali la 3..

Jedwali la 3: Kiolezo cha Bajeti ya Ruzuku ya Kati/Kubwa

Kipengele (Shughuli)	Kizio	Kiasi	Gharama ya kizio (Sh.)	Jumla ya Gharama (Sh.)
Ununuzi wa vitu				
Ununuzi wa vifaa na nyenzo				
Ujira				
Gharama za usafiri				
Posho ya kujikimu kwa				

Mengineyo (tafadhali taja)				
	Jumla			
	Ombi kutoka Mfuko			
	Michango kutoka			
	Mchango wa Mwombaji			

4.0 VIAMBATISHO

Taarifa za ziada za kuongeza ubayana wa maandiko ya miradi zinatakiwa zitolewe kwenye Viambatisho. Taarifa za kuambatisha zinajumuisha muundo wa asasi/ taasisi/ (isipokuwa kwa taasisi za serikali), Jedwali lijengalo hoja yenye mantiki iletayo kukubalika kwa Mradi, nakala ya cheti cha asajili wa asasi (kwa vikundi/asasi/taasisi), barua za udhamini (kwa waombaji binafsi), ramani, barua za udhamini na uthibitisho wa kukubali kutoka kwa washiriki wa mradi, wasifu wa wafanyakazi wakuu na taarifa nyingine zinazohusika. Maandiko yote ya miradi ya utafiti yanapaswa kuonyesha mapitio ya makala na taarifa za marejeo, na kwa maandiko mengine, orodha ya marejeo iwekwe kwenye viambatisho. Kila rejeo linatakiwa liwe na majina ya waandishi, jina la jarida, jina la kitabu, namba ya juzuu, namba za kurasa na mwaka wa kuchapishwa. Kanuni za rejea lazima zifuatwe na kuzingatiwa na waandaaji wote wa maandiko ya miradi.